Majaliwa ataka tathmini uendelevu miradi ya uwezeshaji kaya maskini

Na Vitus Audax, MWANZA

WAZIRI Mkuu, Kassim Mjaliwa, ameuagiza Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) kupitia Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini, kuhakikisha unafanya tathmini na kutoa mapendekezo kwa serikali juu ya upungufu wa kaya maskini nchini.

Majaliwa alibainisha hayo jana jijini Mwanza wakati akikagua maendeleo ya taasisi mbalimbali nchini katika kongamano la nne la ufuatiliaji, tathimini na ujifunzaji.

Alisema takwimu zinaonesha kuwa idadi kubwa ya kaya zinaoneka kuondokana na umaskini kila kukicha, hivyo kuna haja ya mfuko huo kushauri juu ya kipi serikali hususani pale kaya masikini zinapoonekana kupungua.

"Takwimu zinaonesha wengi wame 'graduate', hivyo hali ya umaskini imeshuka. Nini tathimini yenu pengine umaskini unaisha au la," alisema Majaliwa.

Katika hatua nyingine, Waziri Mkuu Majaliwa alisema Rais Samia Suluhu Hassan anaamini katika tathimini na kuwa ni maelekezo yake zifanyike kwa ukamilifu na kila taasisi ya umma ili kuhakikisha Dira ya Taifa ya Maendelo ya mwaka 2025 - 50 inatekelezwa ipasavyo.

Alisema hatua hiyo itasaidia matokeo ya utekelezaji wa dira hiyo yanaweza kupimika mbele ya umma wa watanzania kupitia tathimini na uratibu na kuhakikisha yanaleta manufaa kwa watanzania wote.

Mkurugenzi wa Ufuatiliaji, Tathmini, Mifumo na Mawasiliano wa TASAF, Japhet Boaz, alisema tathmini inasaidia kuona hali ya umaskini ilivyo nchini na kubaini kuwa juhudi za kuondoka hali hiyo na si za kufanya na kuacha.

Alisema licha ya umaskini kuendelea kupunguzwa zinatakiwa juhudi endelevu hasa katika kukabiliana na changamoto kubwa zinazowakabili wananchi.

Alisema mpaka sasa wamefika asilimia nane pekee kati ya kumi za maskini wanaotajwa kuwepo nchini kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022 hivyo juhudi za kuhakikisha maskini wanainuliwa zinaendelea.

"Hatuwezi kusema sasa umaskini umeisha hivyo mpango usitishwe bali lazima uwepo kwani kuna wakati yanatokea majanga na kuipua maskini wapya ambao wanahitaji msaada wa serikali," alisema Boaz.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), William Lukuvi alisema Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali za elimu imeratibu mafunzo maalum kuhusu ufuatiliaji na tathimini kwa maofisa wakuu wa vitengo 781 kutoka ofisi mbalimbali.

Alisema hatua hiyo ni mkakati mkubwa unaolenga kujenga uwezo wa kitaifa wa ufuatiliaji na Tathimini ambao serikali inautambua na kuuthamini.